**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 07 Mei 2001 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Eleza hatua nne zinazomsaidia mwanafunzi kukuza stadi ya kuandika kwa ufasaha.
2. Toa hoja nne kuthibitisha kuwa nyimbo za Kiswahili ni kioo cha maisha ya kijamii.
3. Bainisha sifa nne za mtindo wa barua ya kikazi na ueleze umuhimu wake.
4. Eleza kwa mifano tofauti kati ya semi za methali na nahau katika Kiswahili.
5. Taja mambo manne ya kuzingatia mwalimu anapofundisha insha kwa vitendo.
6. Eleza kwa kifupi vigezo vinne vya kumsaidia mwalimu kupanga malengo mahsusi ya somo.
7. Toa mifano ya tamathali nne za semi na eleza umuhimu wake katika ufundishaji wa Kiswahili.
8. Fafanua tofauti kati ya andalio la somo na shajara ya kazi ya mwalimu.
9. Taja aina nne za kazi za ushairi na eleza nafasi yake katika malezi ya kijamii.
10. Eleza mambo manne muhimu ya kuzingatia katika utayarishaji wa mwongozo wa mitihani.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza namna mbinu ya kazi za vikundi inavyoweza kukuza ushirikiano na uelewa miongoni mwa wanafunzi.
12. Kwa hoja tano, thibitisha umuhimu wa kutumia vitendawili katika kukuza ubunifu wa wanafunzi.
13. Jadili hatua kuu nne za mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ukitoa mifano.
14. Eleza tofauti zilizopo kati ya barua ya magazetini na barua ya kirafiki, ukitoa mifano ya matumizi yake.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sifa tano za zana bora za kufundishia na jinsi zinavyoongeza ufanisi wa mwanafunzi.
16. Kwa hoja tano, eleza manufaa anayopata mwalimu kwa kutoa majaribio ya mara kwa mara darasani.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

17. Jadili mbinu tano ambazo mwalimu anaweza kutumia ili kuongeza hamasa ya wanafunzi katika masomo.

18. Eleza changamoto tano zinazoweza kujitokeza wakati wa kutumia mbinu ya mihadhara katika ufundishaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org